Visit: www.Africona.net/Teacherpizo for Free Past Papers

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

MAHIRI DEVELOPMENT PLATFORM (MADEP)

NAMBA ZA SIMU: 0678827971/0767632301

MTIHANI WA KWANZA WA UTAMILIFU DARASA LA SABA-MACHI 2019

SOMO : SAYANSI

NAMBA YA MTAHINIWA : _____

JINA LA SHULE : _____

WILAYA : _____

MKOA : _____

MUDA : SAA 1: DAKIKA 30

Maelekezo

1. Jaza nafasi wazi hapo juu na katika karatasi ya kujibia.
2. Jibu maswali yote kwa kufuata maelekezo katika kila sehemu.
3. Chagua jibu sahii kisha siliba herufi yake katika karatasi ya kujibia OMR kwa kutumia kalamu ya risasi kuanzia swali 1 hadi 40.
4. Katika swali la 41 hadi 45 jibu maswali kwa kuandika majibu nyuma ya karatasi ya OMR.
5. Hakikisha kazi yako ni nadhifu na safi.

SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA

Chagua jibu sahihi kisha siliba herufi ya jibu hilo kwenye karatasi maalumu ya kujibia (OMR) uliyopewa

1. Viungo gani kati ya hivi vifuatavyo vinahusika na utoaji wa takamwili?
   A. Moyo na mapafu C. Ini na bandama E. Tezi na ini [ ]
   B. Figo na tumbo D. Figo na ngozi
2. Kundi lipi la wanyama kati ya hawa wafuatao linaonesha wanyama wenye uti wa mgongo?
   A. Popo, bata na kuku C. Mjusi, konokono na kenge E. Chura, nyoka na nzi [ ]
   B. Mbuzi, nyoka na panzi D. Jongoo, funza na nyoka
3. Joto husafiri katika maji kwa njia ya:
   A. Mvukizo B. Msafara C. Mnunurisho D. Mpitisho E. Mzunguko [ ]
4. Sehemu ya kike ya ua hujulikana kama:
   A. Pistili B. Ovari C. Chavua D. Stameni E. Staili [ ]
5. Aina gani ya madini husaidia ukuaji na uimarishaji wa mifupa na meno katika mwili wa mwanadamu?
   A. Kalisiamu B. Magnesiamu C. Ayodini D. Fosiforasi E. Chokaa [ ]
6. Wakati wa ujauzito kijusi hupokea chakula na hewa kutoka kwa mama kupitia:
   A. Uterasi B. Plasenta C. Mirija ya falopia D. Ovari E. Urethra [ ]
7. Chembechembe nyekundu za damu hutengenezwa katika:
   A. Haimoglobini B. Tishu C. Mifupa mirefu D. Plasma E. Moyo [ ]
8. Kwa kawaida mtu mzima huwa ana jumla ya meno mangapi?
   A. 28 B. 42 C. 32 D. 53 E. 38 [ ]
9. Mshipa mkuu unaotoa damu kwenye moyo kuipeleka sehemu zingine za mwili hujulikana kama:
   A. Ateri B. Vena C. Aota D. Palmonari E. Vakyuri [ ]
10. Vifuatvyo ni vyakula vya wanga ISIPOKUWA:
    A. Mchele B. Karanga C. Mahindi D. Ulezi E. Mtama [ ]
11. Neva inayounganisha jicho na ubongo hujulikana kama:
    A. Aksoni B. Konjaktiva C. Optiki D. Kornea E. Pupili [ ]
12. Vimelea vinavyosababisha ugonjwa wa malaria hujulikana kama:
    A. Virusi B. Fangasi C. Bakteria D. Plasmodia E. Mbu [ ]
13. Sehemu gani ya mwili wa binadamu inahusika na kuchuja mkojo?
    A. Moyo B. Figo C. Ngozi D. Tumbo E. Ini [ ]
14. Ni aina gani ya vyakula vinafaa kwa mama mjamzito?
    A. Wanga B. Mafuta C. Vitamini D. Kabohaidreti E. Protini [ ]
15. Njia ipi kati ya hizi zifuatazo haiwezi kusababisha maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI?
    A. Kujamiiana D. Kupeana mikono na muathirika wa UKIMWI [ ]
    B. Kuchangia vitu vyenye ncha kali E. Kutoka kwa mama muathirika kwenda kwa mtoto
    C. Kuongeza damu yenye virusi vya UKIMWI
16. Katika sakiti ya umeme alama hii  kilisha kitu gani?
    A. Seli kavu B. Betri C. Fyuzi D. Galvanomita E. Amita [ ]
17. Tabaka la nje la ngozi hujulikana kama:
    A. Endokrini B. Epidemisi C. Melanini D. Demisi E. Endodemisi [ ]
18. Kifaa kipi kati ya hivi vifuatavyo hutumika jotoridi?
    A. Baromita B. Anemomita C. Haigromita D. Themomita E. Kipima mvua [ ]
19. Sehemu ya uzazi ya mwanamke inayooneshwa kwa herufi E katika mchoro ufuatao ina kazi gani?

    A. Kupokea mbegu za kiume D. Kuzalisha mbegu za kike
    B. Kuhifadhi kichanga E. Kusaidia mzunguko wa hedhi [ ]
    C. Kuunganisha ovari na mirija ya falopia

20. Chembechembe ndogo zinazounda maada hujulikana kama:
A. Elementi B. Kampaundi C. Molekyuli D. Atomi E. Tishu [ ]

21. Maji huganda kwa kizingiti cha sentigradi ngapi?
A. Sentigredi 0_0 B. Sentigredi 100_0 C. Sentigrade 1000_o D. Sentigredi 25_o E. Sentigradi 10_0 [ ]

22. Kiumbe yupi kati ya hawa wafuatao hujilinda dhidi ya maadui kwa kujibadilisha rangi?
A. Kinyonga B. Popo C. Mjusi D. Nyoka E. Samaki [ ]

23. Mtu mwenye tatizo la kutoona vizuri vitu vilivyo karibu anaweza kutatua tatizo hilo kwa kuvaa miwani yenye:
A. Lenzi mbinuko B. Lenzi mbonyeo C. Lenzi ya kawaida D. Kioo bapa E. Kioo mbinuko [ ]

24. Sehemu gani katika kamera inafanana na retina katika jicho?
A. Filamu B. Lensi C. Balbu D. Swichi E. Fokasi [ ]

25. Metali ipi kati ya hizi zifuatazo huathiriwa na kutu?
A. Bati B. Zinki C. Zebaki D. Chuma E. Shaba [ ]

26. Mashine imebeba mzigo wa kilo 40 kwa kutumia jitihada ya nyutoni 20. Tafuta manufaa ya kimakenika.
A. 800 B. 20 C. 2.0 D. 0.2 E. 0.002 [ ]

27. Ugonjwa upi kati ya magonjwa yafuatayo unatokana na ukosefu wa madini joto?
A. Malaria B. Kifaduro C. Upungufu wa damu D. Rovu E. Matege [ ]

28. Kiumbe yupi kati ya hawa wafuatao ni amfibia?
A. Mamba B. Binadamu C. Chura D. Kinyonga E. Samaki [ ]

29. Tezi inayodhibiti ukuaji wa mwili wa binadamu hujulikana kama:
A. Pituitari B. Adrenali C. Kongosho D. Ovari E. Parathairoidi [ ]

30. Sehemu iliyooneshwa kwa herufi **B** katika kielelezo kifuatacho huitwa:



A. Kiwambo
B. Saitoplazimu
C. Nyukiliasi [ ]
D. Kiini
E. Utando wa seli

31. Kisayansi uwezo wa kufanya kazi hujulikana kama:
A. Nishati B. Nguvu C. Kani D. Momemtamu E. Msukumo [ ]

32. Sakiti ya umeme iliyokamilika inakuwa na betri, waya, balbu pamoja na:
A. Chaja B. Nguzo za umeme C. Transfoma D. Swichi E. Tochi [ ]

33. Sauti iliyoakisiwa hujulikana kama:
A. Kelele B. Mawimbi C. Mawasiliano D. Mwangwi E. Mtetemo [ ]

34. Gesi inayosaidia moto kuwaka ni:
A. Kabonidaiyoksaidi B. Oksijeni C. Kabonimonoksaidi D. Haidrojeni E. Naitrojeni [ ]

35. Homoni inayodhibiti kiasi cha sukari katika mwili wa binadamu hujulikana kama:
A. Amilesi B. Glukosi C. Insulini D. Ayodini E. Pepsini [ ]

36. Sehemu inayowakilisha na herufi **A** katika mchoro ufuatao huitwaje?



A. Retina D. Mishipa [ ]
B. Mboni E. Kope
C. Kornea

37. Sayari ipi kati ya hizi zifuatazo hujulikana kama nyota ya asubuhi?
A. Venasi B. Dunia C. Yuranusi D. Neptuni E. Jupita [ ]

38. Upungufu wa virutubisho muhimu vinavyohitajika mwilini hujulikana kama:
A. UKIMWI B. Utapiamlo C. Malaria D. Kwashakoo E. Magonjwa [ ]

39. Kwa kawaida mmeng'enyo wa chakula mwilini huanzia kwenye:
A. Tumbo B. Mdomo C. Koromeo D. Utumbo mpana E. Utumbo mwembamba [ ]

40. Kutu hutokea kutokana na muunganiko wa kikemikali baina ya chuma, Oksijeni na:
A. Kabonidaiyoksaidi B. Maji C. Hewa D. Mvuke E. Ukungu [ ]

SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Jibu swali la 41-45 kwa kuandika majibu sahihi kwenye karatasi ya kujibia uliyopewa

41. Kitendo cha mmea kukua kuelekea mwanga wa jua hujulikana kama_____

42. Badili nyuzi 122 za Fareinheiti kuwa nyuzi za sentigredi

43. Tafuta thamani ya X katika mchoro ufuatao



44. Sehemu ya ubongo inayoratibu matendo ya hiari hujulikana kama_____

45. Taja jina la sehemu inayowakilishwa na herufi N katika mchoro ufuatao